GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. **246** J/D/Awwal-Akhirah **1446** AH Disemba– **2024** Fatah **1403** HS BEI TSH 800/=

ZIARA YA AMIR SAHIB

NA JALSA SALANA YA MKOA WA IRINGA

Na; Twaha Nyange

Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Mkoa wa Iringa, Kwa Fadhili za Mwenyezi Mungu tarehe 08&09/11/2024 tulijaaliwa kufanya Mkutano wa Mwaka (Jalsa Salana) ambao ulihudhuriwa pia na Kiongozi wetu mkuu wa Tanzania, Amir na Mbashiri mkuu wa Tanzania Maulana Sheikh Khawaja Muzafar Ahmad. Wito wa kufanya Jalsa Salana ya Mkoa wa Iringa ulitolewa na Amir Sahib mara baada ya kumaliza Jalsa salana ya Kitaifa kwa kuwa alipanga ziara ya kutembelea mkoa wetu. Hivyo, bila ajizi tuliupokea wito huo kwa kusema tumesikia na



tunatii. Licha ya kuwa maandalizi ya Jalsa yalikuwa ndani ya mwezi mmoja tu kati ya tarehe husika za Jalsa ya Mkoa na Jalsa ya Kitaifa ilipokwisha.

Amir Sahib na ujumbe wake aliwasili Iringa siku ya Alhamisi majira ya saa kumi na mbili jioni (12:00) akiambatana na Sheikh Abdulrahman Ame, Sheikh Asif Mahmood Butt na Sheikh Asif Raza Sahib Ujumbe wake ulilakiwa na Wanajamaat waliokuwepo Makao makuu ya Mkoa eneo la Gangilonga Iringa.

Siku ya Ijumaa (08/11/2024) majira ya saa tatu na dakika ishirini asubuhi (3:20), Amir sahib pamwe na ujumbe wake na viongozi wengine wa Jamaat wa Mkoa wa Iringa waliambatana na kutembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa Mh, Peter Joseph Serukamba.

Awali Amir Sahib alimweleza

UK. 05

Ziara ya Amir na Mbashiri mkuu Tanzania, Kanda ya Kusini Magharibi Mbeya.

Na; Mwandishi wetu.

Mkoa wa Mbeya upo umbali wa Kilomita 822 kuelekea kusini-magharibi kutokea jijini Dar es Salaam,

Mkoa huu wa Mbeya una wilaya sita, nazo ni Mbeya, Tukuyu, Kyela Chunya na Mbarali. Huu ni Mkoa wa 31 wa Tanzania, wakazi wake ni milioni mbili na eneolake ni kilomita za mraba 35,954. Mkoa wa Mbeya una makabila makubwa matatu, Nyakyusa, Safwa, Sangu, na inapakana na nchi tatu za Malawi, Zambia, na Kongo.

Mwanzo wa Ahmadiyya Mkoa wa Mbeya

Jamaat ilianza katika Mkoa wa Mbeya mwaka wa 1983 na Dk. Iddi Ibrahim Mwanga (Marehemu), Bwana Hasan Molly Sahib (Marehemu) na Bwana Ambari Mpulaki Sahib, Kituo cha sala kwa mara ya kwanza kilikuwa nyumbani Kwa Dr. Iddi Ibrahim Mwanga. Kisha baada ya muda fulani kilihamishiwa katika nyumba ya Mzee Hassan Moli Sahib na baadaye Jamaat ilipata nyumba mtaa wa Jakaranda.

Mwl Isa Sahib alikuwa Mwalimu, baadaye Sheikh Farid Ahmad Tabassam Sahib kutoka Pakistani alikaa kama mbashiri mwaka 2004, baada yake Sheikh Mubarak Ahmed ambae ni marehemu, Sheikh Khawaja Muzaffar Ahmad Sahib, ambaye sasa ni Amir na mbashiri mkuu anayeongoza Tanzania, alikaa hapa kama mbashiri mwaka wa 2006, Kisha Sheikh Basharat Rahman Sahib, kisha kutoka 2014 hadi 2022 Sheikh Karimuddin Shams Sahib na sasa Sheikh Muhammad Daud Bhatti anaeishi katika eneo la msikiti Masjid Nasir.

Maelezo ya ziara ya Mheshimiwa Amir na Mbashiri mkuu Sheikh Khawaja Muzaffar Sahib

Jumatatu,

11, 2024, baada ya ziara ya Mkoa wa Iringa, jioni baada ya sala ya Al-Asr, Mheshimiwa Khawaja Muzaffar Ahmed, Amiri na Mbashiri mkuu anayesimamia Makao Makuu ya Tanzania, Aliwasili Masjid Nasir Mkoa wa Mbeya, ambapo Sheikh Muhammad Daud Bhatti, alimpokea vyema na watu wa eneo hilo pia walimpokea vyema.

Baada ya sala ya Maghrib na Isha, Amiri na Mbashiri mkuu alipitia mpango wa ziara katika mkoa huo ya siku ya pili, ilipofika Jumanne Novemba 12, 2024, matawi mbalimbali ya mkoa yalitembelewa na Msafara huu kwa kushiriki katika Jalsa za Malezi. Asubuhi baada ya ratiba ya sala na kifungua kinywa, tulifanya maombi kisha safari iliianza na Mheshimiwa Amir Sahib, Naib Amir Sheikh Abdul Rahman Ame Sahib, Sheikh wa Mkoa wa Mbeya Sheikh Muhammad Daud Bhatti Sahib, Rais wa Mkoa wa Mbeya Munibullah Marunda, pia upande wa Lajna walikuwepo viongozi wa Kitaifa Naibu Sadri Lajna Taifa Bi. Naomi Mashingo, Katibu Lajna Taifa Bi Alfa Kaluta pamoja na Sadri Lajna Mkoa wa Mbeya Bi. Aisha Idrisa aliwakilisha Mkoa wa Mbeya.

Na mfanyakazi wa MTA alihusika Bw. Mohammed Higiro.

Mpango huo ulianza kutoa

UK. 03

MATUMAINI YA AMANI DUNIANI >UK .04

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

UTAMU WA HISTORIA

Unaweza kuamini na huu ndio utamu wa Historia. Haifichi kitu, inajaribu kuweka mambo bayana. Tumetoka mbali. Tunao wajibu mkubwa kumshukuru Allah tukijua tulipotoka na tanuru la mateso tulilopitia tutaongeza maombi na shukrani kwa Allah. Tumetoka mbali na kutendewa madhila. Kipo kipindi katika nchi yetu watu waliposimama kwenye mimbari na kutangaza Kuruani Tukufu tuliyotafsiri katika kiswahili ina juzu thelathini na moja. Misahafu tuliyochapisha mingi imenunuliwa na wao. Hatujapata hata mmoja aliyetuletelea ushahidi kuwa tafsiri yetu ina sura thelathini na moja. Historia imetulinda na kututetea. Wengine walipayuka kuwa adhana yetu ni tofauti tunaongeza Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (as) .

Allah Ametujaalia tumejenga msikiti mkubwa na mzuri na vipaza sauti vinasaidia kuwasuta wale wanaotusingizia. Kuhusu hilo wala hatuna haja ya mabishano, mwenye masikio anasikia. Tulitukanwa na kubezwa kuwa sisi ni makafiri kwa sababu hatuamini Nabii Isa (as) yuko mbinguni. Sisi tuliendelea kutoa Aya za Kuruani tukufu na Hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Hivi leo wamegwaya-wanasema kama amekufa au hakufa haina maana yeyote. 'Si kweli' sawa na wao Nabii Isa (as) atakuja amevalia kijeshi huku akiuwa nguruwe wa watu na kupora misalaba. Watu wenye busara wamekwisha anza kurudi nyuma na kugundua kupotea kwao. Wanakiri kuwa Nabii Isa (as) ameonja mauti.

Upo wakati hatukuruhusiwa kuingia katika misikiti na tukiingia basi fatwa ni kuisafisha kwani imechafuliwa. Wala hawakuruhusiwa kusali nyuma yetu. Ama kweli siku zenu za baadae zitakuwa bora, kwa hivi sasa hakuna anayekuuliza ikiwa wewe ni Ahmadiyya au la! Na waliokuwa wanaogopa misikiti yetu wanajaa na kusali nyuma na imamu Ahmadiyya. Hapana shaka ukweli ukifika uongo unatoweka. Hivi leo wanajazana katika Masjid Salaam Dar es Salaam, Dodoma na misikiti mingine yetu nchini. Upo wakati tulisingiziwa kuwa Hija yetu ni kwenda Qadian, sasa hivi tunakwenda hata na taasisi za kiislam. Nasi tunamshukuru Allah kuwatoa kwenye giza na kuwaleta kwenye mwanga.

Assalam Alaikum ambalo ni agizo la Allah wao waliliwekea mipaka. Waahmadiyya wakitoa salaam usiitikie. Katika hili tumeendelea kuwatolea salaam bila kuchoka au kukata tamaa, hivi leo wanapokea salaam zetu. Lakini tumekwenda zaidi ya hapo na kuwafundisha kuwa sio dhambi kwa akina Mama kutoa au kupokea Assalam Alaykum, kwao ilikuwa hairuhusiwi kwa kina Mama kutoa Salaam. Alhamdulillah funzo hili sasa limeshika, sasa hivi ni Assalam Alyakum kwenda mbele. Salaam ya kishindo ambayo haitasahaulika ni ile iliyotolewa katika viwanja vya Jangwani. Umati uliokuwa umefurika na aliyekuwa anahutubia ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kabla ya hotuba walipewa zawadi waliotoa michango ya kujenga ofisi ya makao makuu ya chama Dodoma. Jumuiya ya Ahmadiyya ilikuwa ya kwanza kuitwa. Sheikh Muhammad Munawar aliinuka na alipofika kwa waheshimiwa waliokuwa mezakuu Mwalimu Nyerere, Sheikh Abedi Amani Karume, sheikh Thabiti Kombo. Akatoa Assalam Alaykum wakaitikia woote na uwanja mzima ukalipuka kwa Waaleikum Salaam warahmatullah wabarakatuh.


Ukiona kiangazi ujue masika yako karibu. Tumepitia kipindi cha kiangazi na tulisikia harufu ya Masika. Allah Atujaalie tufaidike na Masika hayo ambayo daima hutupatia mvua ya neema kutoka kwa Allah.



QUR'AN TUKUFU

154. Enyi mlioamini, ombeni msaada kwa subira na Sala; bila shaka Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wanaosubiri. *Sura Al-Baqara 2:154*

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اسْتَعِيْنُوْا بِالصَّبْرِ وَالصَّلٰوةِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ مَعَ الصّٰبِرِيْنَ ۝



NUKUU YA HADITHI

Hadhrat Suhaib[ra]. Anasimulia kuwa Mjubme saw wa Allah alisema: "Ya ajabu mambo ya mumini. Mambo yake yote yana heri ndani yake. Nayo hajaaliwii mwingine yeyote minghairi yake. Ikimfikia furaha yoyote hushukuru, inayokuwa heri kwake, walau ikimpata udhia wa aina yoyote, husubiri, nayo pia huwa heri kwa ajili yake. "
Sahihi Muslim, Mlango utawa na mambo mepesi, kifungu cha mumini mambo yake yote ni heri.



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Subira ndiyo inayozishinda nyoyo.

Maneno matakatifu ya Sayidina Ahmad as. Masihi Aliyeahidiwa:
Thibitisheni kwa mfano wenu uliotakata na kwa mwenendo wenu bora kwamba mmeshaimarika juu ya njia takatifu. Angalieni, nimetumwa kwa jambo hili kwamba niwakumbushe mara kwa mara kuwa mjiepushe na kila ufisadi, na sehemu za magomvi/uharibifu. Onyesheni subira hata mkitukanwa. Lipezeni uovu kwa wema. Na mtu yeyote akipenda/akiwa tayari kufanya ufisadi, yawafaa kuondoka sehemu kama hiyo. Na jibuni kwa upole. Nakuambieni kweli kweli kuwa msiache subira kamwe. Silaha ya subira ni ya hivi kwamba mzinga hausaidii vile ambavyo inasaidia subira. Subira ndiyo inayozishinda nyoyo. Bila shaka kumbukeni kuwa yanisikitisha mno ninaposikia kwamba mtu fulani akiwa wa Jumuiya hii amegombana na mtu fulani. Siupendi kabisa mwenendo huu, na hata Mwenyezi Mungu hataki kuwa Jumuiya itakayokuwa mfano miongoni mwa dunia nzima ikanyage njia isiyo njia ya taqwa, bali nawaambieni na hili pia kwamba Mwenyezi Mungu Analiungia mkono/penda jambo hili kiasi ya kwamba lau mtu yeyote asipoonyesha subira na uvumilivu/ustahmilivu akiwa miongoni mwa jumuiya hii, basi akumbuke kuwa hayumo ndani ya jumuiya hii.

(Malfuzat, Jalada 6, uk. 354-355, chapa 2022)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

Ziara ya Amir na Mbashiri mkuu Tanzania, Kanda ya Kusini Magharibi Mbeya.

Kutoka uk. 01

Ubaruku, ambalo lipo takriban kilomita 130 kutoka makao makuu Mbeya Mjini. Tawi hilo lipo Mashariki mwa makao makuu ya Mbeya.

Tawi Hilo Lilianzishwa mwaka 2019 kufuata juhudi za Tablighi zilizoanza tangu Mwaka 2017 na Mwalimu Makarani Hamza Balama Makarani Sahib.

Baadaye, msikiti ulijengwa tawi la Ubaruku na likapewa jina la Bait-ul-Khabir wakati wa Uongizi wa Sheikh Kareemuddin Shams Sahib.

Katika tukio Hili la Tarbiyyat Jalsa, Tawi la Ubaruku lilihudhuriwa na watu Arobaini na nane (48) kwenye Jalsa ya Malezi tawini hapo. Msafara wa Mheshimiwa Amir Sahib ulifika Ubaruku baada ya safari ya saa moja na nusu, na baada ya sala ya Adhuhuri na Alasiri tukio lilianza kwa usomaji wa Qurani Tukufu na tafsiri yake, ambayo iliwasilishwa na Da'in Mwalimu Saleh Umar Sahib, ikafuata na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya ndani ya Tawi la Ubaruku, Ndugu Rupiana Konga Sahib alielezea historia ya awali ya Ahmaddiyya Tawi la Ubaruku, Baada ya hapo, Mheshimiwa Naib Amir Sahib Sheikh Abdul Rahman Ame Sahib alitoa hotuba fupi juu ya Majukumu ya mume na mke katika maisha ya familia, kisha Amir na Mbashiri mkuu Sheikh Khwaja Muzaffar Ahmad akatoa Hotuba juu ya Majukumu ya Mwajamaat kwa nidhamu ya Ukhalifah wa Ahmadiyya, akifuatiwa na Mwalimu Hamza Makarani Alitoa hotuba fupi akifuatiwa na Hotuba ya Rais wa Mkoa Munibullah Marunda, kisha Sheikh wa Mkoa Mohammad Dawood Bhatti alimshukuru Amir na Mbashiri Mkuu, na Baadae Amir na Mbashiri Mkuu walipanda mche wa mti wa matunda na jiwe la msingi la Nyumba ya Mwalimu liliwekwa na pipi ziligawiwa miongoni mwa watoto katika hafla hii na baada ya sala ya pamoja na picha ya pamoja chakula kilitolewa kwa marafiki.

Baada ya swala ya Maghrib na Isha, Wajumbe wa Taifa Lajna na Sadri Lajna Mkoa wa Mbeya walifanya kikao na Lajna wa Tawi hilo pia walikutana siku hiyo hiyo.

Mheshimiwa Amir Sahib Alifanya mkutano wake na Jumla ya mahudhurio ya programu hii yote ilikuwa 75.

Katika siku ya pili, Jumanne, Novemba 13, Swala ya Alfajiri iliongozwa na Amir Sahib na Dars al-Qur›an, lenye anuani ya Baraka za Kujitolea Mali, lilitolewa na Rais wa Mkoa Ndugu Munibullah Marunda Sahib.

Baadaye, baada ya kifungua kinywa, akiwa njiani kurudi Mbeya Mjini, alitembelea tawi la Chimala na Ihahi Jamaat.

Mahali paitwapo Masasi Chimala ambapo Kuna nyumba ya mwalimu, anapoishi Mwalimu Hamza Makrani Sahib. Amir Sahib alisimama, na kukagua nyumba hiyo na mazingira yake, Kisha alitoa maelekezo mbalimbali ya kufanyiwa kazi.

Jamaat ya Chimala ilianzishwa mwaka 2018.

Kisha Amir Sahib aliendelea na safari ya kuelekea Tawi la Ihahi.

Tawi la Ihahi lilianzishwa mnamo mwaka 2021 na Msikiti ulijengwa hapa mwaka 2022 wakati wa wakati wa Sheikh Karimuddin Shams Sahib Jina la msikiti huu ni Baytul Karim. Msafara wa Amir Sahib ulifika Ihahi saa 5 kamili. Jalsa ya Tarbiyyat ilianza mara tu alipowasili Amir sahib na Msafara wake.

Kikao kilianza kwa usomaji wa Quran iliyosomwa na Mwalim Nazir Ramadhan Sahib (Dayyan ilallah) anaehudumia katika Tawi hilo. Baadae ya shairi lililosomwa na Mwl Makarani Hamza Kisha Rais wa Tawi Bwana Rashid Mgadagu alitoa historia fupi ya Jamaati ya Ihahi, na baada ya hapo Naib Amir alitoa hotuba juu ya baraka za Ukhalifa hotuba ambayo ilisisimua Sana wasikilizaji. Baada ya hapo, swala ya Adhuhuri na Alasiri ikaswaliwa, baada ya hapo lilifanyika zoezi la upandaji mti na kuweka Jiwe la msingi la nyumba ya Mwalimu, na kufuatiwa na maombi ya pamoja kwa ajili ya mti wenye matunda. Picha za pamoja zilipigwa ambapo Amir Sahib na Msafara wake, wanajamaat na wageni wote walioshiriki jalsa hiyo. Baadae Amir Sahib aligawa pipi miongoni mwa watoto.

Katika hafla hii, wawakilishi wa Kanisa, wawakilishi wa serikali ya Kijiji, wajumbe kutoka Uongizi wa Chama cha CCM, Mwalimu mkuu wa shule ya Ihahi, na wawakilishi wa Bakwata na Sunni pia walishiriki na rafiki mmoja katika wageni hao aliomba kufanya Baiat baada ya kuathirika na kikao hicho, Alhamdulillah. Hapa pia, jumla ya mahudhurio ilikuwa 82.

Baadaye, chakula kilitolewa kwa marafiki.

Baada ya kuondoka katika Tawi la Ihahi majira ya Alasiri ya Mheshimiwa Amir Sahib alifika Tena kwenye nyumba ya Mwalimu Masasi-Chimala na pamoja na msafara wake, ambapo alikula chakula cha mchana na msafara huo baada ya kutoka huko, alitembelea Tawi la Ilongo. Alifika hapo saa 12:00 jioni akikaribishwa na Mwalimu wa eneo hilo Mwl Sabili Miraji Simba (Daiyan ilallah) na baadaye Mheshimiwa Amir alikagua msikiti na nyumba ya Mwalimu na kutoa maagizo kadhaa, kisha akafanya kikao kifupi na Wanajamaat wa hapo, ambapo alipata nafasi ya kuzungumza mambo machache na wanajamaat akihimiza wanajamaat kuwa mfano mwema Kwa watu. Washiriki wa Kikao Kwa Tawi la Ilongo walikuwa 33. Kisha Amir Sahib alipiga picha ya pamoja na Wanajamaat wa Ilongo, na kuanza safari ya kurudi Mbeya Mjini, Muda wa Insha msafara wa Mheshimiwa Amir Sahib ulikuwa umeshawasili Mbeya mjini na kukusanyika kwa ajili ya Swala ya Maghrib na Isha.

Tarehe 14 Novemba, Alhamisi, Makao Makuu Mbeya Mjini.

Kulikuwa na programu ya Jalsa ya Tarbiyyat huko Mbeya Mjini, Msingi wa Jumuiyya ya Ahmaddiyya uliwekwa na marehemu Ndugu Iddi Ibrahim mnamo 1983. Tawi hili lina Jumla ya wanajumuiya 102.

Sala ya Tahajjud iliongozwa na Naib Ameer Sheikh AbdulRahman Ame Sahib,

Sala ya Alfajiri iliongozwa na Mheshimiwa Amir Sahib na Darsa la Baraka za Maisha ya Kujitolea waqf, lilitolewa na Sheikh wa Mkoa wa Mbeya Muhammad Dawood Bhatti.

Baada ya hapo saa 2:30 asubuhi Mheshimiwa Amir Sahib, Rais wa Mkoa wa Mbeya na wawakilishi wa , walikwenda Kwa mkuu wa Wilaya Halmashauri ya Mbeya Mjini kwenye ofisi yake.

Mkutano huu ulifanyika katika mazingira ya kupendeza.

Mheshimiwa Amir Sahib na wawakilishi wa Jumuiya walikuja kwa ajili ya mkutano ulioratibiwa, na Baada ya Mazunguzo machache Mheshimiwa Amir Sahib alimzawadia mkuu wa Wilaya Quran Tukufu ya Kiswahili na kitabu Cha Mgogoro Wa Dunia na zawadi ya shajara(Diary)

Baada ya Kikao hiki huu, Amir Sahib alirejea Masjid Nasir.

Saa 5:30 asubuhi, kilifanyika Kikao Kati ya Amir Sahib, walimu, na viongozi wa matawi wa kanda, kikao ambacho kiliendelea hadi wakati sala ya Adhuhur ambazo Sala ya Adhuhur na Alasiri zilisaliwa Kwa kuunganishwa.

Jalsa ya Tarbiyyat ilianza ambapo Mwalimu Hamza Makarani alisoma Quran Tukufu Na tafsiri kisha shairi likasomwa na katibu wa Tawi la Mbeya Mjini Ndugu Jalaluddin Mbawala Sahib, baada ya hapo Rais wa Mkoa Ndugu Munibullah Marunda Sahib alitoa historia fupi ya Jamaat ya Mbeya Mjini. Na akashukuru kwa kuwasili kwa Mheshimiwa Amir Sahib katika eneo hilo. Baada ya hapo, Naib Amir Sahib alizungumza juu ya Maana ya Ukhilafah na majukumu na wajibu wetu wa maisha ya familia, baada ya hapo chakula cha mchana kililiwa na kupiga picha ya pamoja na marafiki. Hapa pia viongozi Lajna Imailah Taifa wakifanya kikao na wanaLajna wa Mbeya Mjini na viongozi wa Mbeya Alhamdulillah, mpango huu ulifanikiwa kama programu nyinginezo jumla ya mahudhurio yalikuwa 90.

Mambo ya kuvutia katika ziara hii.

1. Mheshimiwa Amir Sahib ametembelea Mbeya Kwa mara ya Kwanza Baada ya Kushika ofisi ya Uamiri.

Kwa mara ya mwisho Mbeya ilitembelewa na Amiri mwaka wa 2019 na Mheshimiwa SheikhTahir Mahmood Chaudhry.

Mheshimiwa alikuwa ametembelea, Misikiti miwili na mwalimu mmoja.

2. katika ziara hii Ukarabati wa nyumba ulipitiwa upya

3. Jiwe la msingi la nyumba mbili za walimu liliwekwa.

4. Baada ya miaka 19, Mukram Amir alikuja katika eneo hili akiwa ni Amir na Mbashiri Mkuu

5. Alikutana na marafiki wa zamani

6. Baiat ilipatikana katika ziara hii Alhamdulillah.

7. Katika programu zote za ziara, Idadi ya washiriki ni 285.

Wassalam.

Maelezo ya Sheikh Muhammad Daud Bhatti Sheikh wa Mbeya

2024/11/18

MATUMAINI YA AMANI DUNIANI

Mahojiano na Khalifatul Masih wa V[atba] yalifanywa na Lat Blaylock, Mhariri wa RE today na wakili maarufu wa RE, mahojiano yalifanyika siku ya jumatano 27 February 2023 Masjid Mubarak-Tilford Surrey)

Mtukufu Khalifatul Hazrat Mirza Masroor Ahmad ni Khalifa wa V wa jumuiya inayopatikana duniani kote ya Ahmadiyya. Ilikuwa ni bahati na heshima kubwa kwangu kuwa na mahojiano naye, mwaka 2023 katika Masjid Mubaraka Tilford surrey. Mahojiano haya yatakuwa ya faida kubwa sana kwa wanaofanya mitihani ya GCSE na mitihani mingine kuhusu somo la Islam na vipengele vyake.

Swali: Gazeti la RE today linasomwa na waalimu, nawe ulikuwa mkuu wa shule mbili huko Ghana. Ukiwa Mwalimu ni njia zipi ulizozitumia kufundisha misingi ya dini ya Islam?

Jibu: Shule mbili nilizoziongoza huko Ghana zilikuwa ni za kisekula. Nilipokwenda katika shule hizo walikuwa wanafundisha elimu ya biblia nami nikaanza kufundisha elimu kuhusu Islam. Katika mwaka wa kwanza watoto wote wakristo na Waislam walifanya vizuri katika somo hili. Matokeo hayo yaliwapa msukumo wanafunzi wakristo wachukue somo hili. Vijana wakifundishwa vizuri dini, mafunzo haya yanawasaidia sana katika maisha yao. Zaidi ya asilimia 80 ya wanafunzi wetu walikuwa wakristo. Ile asubuhi kabla ya kuingia darasani yalifanyika maombi sawa na wakristo na maombi sawa na waislam. Kwa njia hii wanafunzi walielewa dini hizi mbili na waliweza kuelewa uvumilivu wa dini ya Islam.

Swali: Ningependa kujua ulivyoshughulikia elimu ya wasichana.
Jibu: Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alisema kila Mwislamu wa kike au wa kiume lazima apate elimu.
Alitufundisha pia kuwa nusu ya elimu ya dini ingepatikana kutoka kwa mke wake Aisha (ra). kuna hadithi nyingi zilizosimuliwa na Bi. Aisha (ra). Baada ya kifo cha Mtukufu Mtume Muhammad (saw) Bi Aisha aliendelea kujibu maswali waliyokuwa nayo masahaba. Yeye aliwapa uzoefu aliokuwa amepata kutoka kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Wanawake wenye elimu wanaweza kuwafundisha akina Baba, wasichana lazima wapewe elimu nzuri, kwa njia hii watoto watakuwa ni wenye faida kubwa kwa jamii. Katika jamaat yetu asilimia 99 ya wanawake na hata iwe katika nchi zinazoendelea wanapata elimu sawa na maana ya elimu katika jamii zao kwa mathalani katika Pakistan tunasema aliyesoma awe amepata elimu ya Sekondari. Jamaat yetu inatoa kipaumbele kwa elimu hata katika vijiji ambako ni vigumu elimu kupatikana.

Swali: Umesisitiza katika wajibu kama Khalifa umuhimu wa amani. Ni katika njia zipi unamuona Mtume kuwa ni mtu wa amani na mleta amani).
Mtukufu Mtume[saw] alipohama kutoka Makka kwenda Madina, alifanya mkataba baina ya waislam na wasio waislam ili waunganike katika jamii moja na alisema kila dini ipewe uhuru. Alitambua kuwa waislam, wayahudi, wakrsito watu wa kitabu wangeweza kuja pamoja katika mambo yanayowahusu na wafanye kazi pamoja wakitambua kuwa wote ni viumbe wa Mwenyezi Mungu na wafanye amani itamalaki duniani. Sasa kama haya ndiyo Mtukufu mtume Muhammad (saw) aliyotekeleza na kwamba hakuna anayeweza kutekeleza mafundisho ya Kuruani Tukufu kuliko yeye, Yeye alituonesha mfano ulio bora kabisa. Mada hii imeelezwa katika vitabu nilivyopendekeza.

Swali: Waalimu wa RE hukuta katika magazeti ya Uingereza picha isiyoridhisha juu ya Islam. Umejitahidi katika njia nyingi kuwahimiza waislamu wawe madhubuti lakini wapole kwa wale wanaoshambulia Islam. Nini ushauri wako kwa waalimu wanaotaka kujenga maelewano miongoni mwa dini?
Jibu: Mafundisho ya dini tukufu ya Islam yanapatikana katika Kuruani Tukufu, haya ndiyo tunayosoma na kujaribu kutekeleza. Pili ni suna-Mwenendo mfano wa Mtume Mtukufu saw hapa tunapata mifano ya kufuata. Tatu, kuna hadithi ambazo zilisimuliwa baadae na baadhi ya masahaba. Kuna vitabu sita mashuhuri vya Hadith. Kama kuna mkanganyiko katika Hadithi basi Kuruani Tukufu inapewa kipaumbele. Tunajitahidi kufuata mafundisho sahihi ya Islam na kuwafikishia wengine. Ikiwa waalimu wataeleza haya kwa wanafunzi wao, basi hayo yatawakilisha mafundisho sahihi ya Islam. Mafundisho lazima yadhihirishwe kwa vitendo na waislam. Kwa njia hiyo picha mbaya inayojitokeza kuhusu Islam itatoweka. Hivi ndivyo tulivyofanya na tumetambuliwa na wasio waislamu Uingereza, Merikani, Afrika na kwingineko sisi waahmadiyya tunajitahidi kutekeleza mafundisho yote ya Islam na ndio maana sisi sio wale wa siasa kali.
Tunafuata sheria za nchi na tunajitahidi kusitawisha amani katika jamii yetu, mafundisho hayawezi kufanya kila kitu, inakubidi kuona mifano. Tunaona ya kwamba dini zote zina mafundisho mazuri, lakini mafundisho hayo hayafuatwi na wafuasi wa dini hizo.

Swali: Umezungumza juu ya umuhimu wa maisha ya kiroho, kumuabudu Allah na kujisafisha nafsi. Ningependa kujua vijana wa hivi leo wanapataje utamu wa sala na kuwepo kwa Mwenyezi Mungu ni upi ujumbe wako kwa vijana kuhusu vipengele tofauti tofauti vya Islam?
Jibu: Kama hujapitia kitu huna kwa njia yoyote ile au huna uzoefu huwezi kukiamini. Tunadai kuwa Islam ni dini ya kweli ambayo inaweza kuwaleta binadamu karibu na Muumba wake. Kama husali sala tano kila siku kama inavyofundisha Islam au husomi Kuruani Tukufu na Kuruani Tukufu inawaonya watu wa aina hiyo kuwa sala zao watarudishiwa kwani matendo yao ni kinyume na mafundisho. Mwislamu wa kweli kama anasali basi inabidi kutimiza haki anazotakiwa kuwatimizia binadamu. Kuruani Tukufu inasema Mwenyezi Mungu ni Rabbal Alameen, Mtoaji na Ambaye Anaupa uzima wakiwemo waislam, wayahudi, wahindi na wengineo. Na kama yeye ni mwingi wa ukarimu kwanini sisi tuwanyime watu wengine haki zao? Tukitimiza wajibu miongoni mwetu na kumuabudu Allah kwa njia hiyo tunaweza kuongeza kiwango chetu cha Taqwa na kutengeneza khulka zetu. Na haya ndio tunayoyahitaji hivi leo.

Swali: Napenda kukuuliza juu ya msimamo wako kuhusu malengo ya mambo yanayohusu tabia nchi hususani kwa nchi masikini, Islam ina msimamo gani kuhusu maswala hayo?
Jibu: Allah Ametengeneza ulimwengu na Yeye ndiye mwingi wa Rehema na ndiye mtoaji wa maisha kwa dunia. Kuruani Tukufu inasema Yeye ndiye anayetoa chakula kwa wanyama na binadamu pia. Kama tumevuruga mizani ya maumbile kwa kukata miti na kuongeza hewa ya kaboni na mambo mengine mengi na kama hatutafuti tiba kwa hayo yote tuliyofanya kuvuruga mizani basi ni sisi tunaohusika na hayo yote yanayotokea. Nina imani kuna uwezekano wa kupata chakula kingi duniani. Kuna ardhi kubwa ya kuzalisha chakula Afrika, Amerika ya Kaskazini, Amerika ya Kusini na Asia. Tukipendana na tukampenda aliyetuumba ni wajibu wetu na kwa viumbe wote wa Allah kuweza kujilisha, kuzalisha chakula zaidi na kutoruhusu mtu yeyote kufa kutokana na njaa.

Kama tuna chakula cha ziada hivi sasa na tunakitupa bila kuwapa wale walio katika umasikini na hii inatokana na kutowajali watu wengine. Lakini kama nchi tajiri zinatimiza wajibu wao bila shaka tunaweza kuinusuru dunia. Mafundisho ya Islam ni kwamba uoneshe huruma kwa wengine, Islam haisemi ufuate itikadi ya kijamaa, inachosema tuwe waangalifu katika kumpatia kila binaadamu chakula. Jirani yako ana haki kutoka kwako na sio jirani mnaoishi mtaa mmoja maana ya jirani ni pana sana. Majirani ni wale wanaofanya kazi pamoja na wale unaosafiri nao. Hivi ndivyo unavyoweza kuinusuru dunia sio tu kutoa chakula bali kujenga amani. Kama unakata miti mahali pamoja basi tupande miti mingi mahali pengine. Binaadamu watumie elimu yao kuleta maendeleo chanya. Tunazungumza kwa matumaini makubwa ingawaje watu wengine matumaini yamepungua tusikate tamaa.

Swali: Jamaat Ahmadiyya mara kwa mara wanakutana na uhasama na mateso na ninaelewa kuwa na wewe umeyapitia hayo. Unasemaje juu ya hali ya Waahmadiyya kwa hivi sasa katika mstakabali mzima wa

Endelea Uk wa 5..

MATUMAINI YA AMANI DUNIANI

Kutoka Uk> 04

Islam. Upi uwezekano wa kukubaliwa?
Jibu:Sisi kazi yetu ni kuhubiri na huwezi kupata shabaha yako kwa mda mchache. Manabii hawa hupata ufaulu wakati wa maisha yao na kwa hakika kuna wakati ilichukua miaka mingi. Tuna imani kuwa kadri miaka inavyokwenda tutakubaliwa. Tunaona mwaka hadi mwaka miongoni mwa waislam na wasio waislam wakijiunga na Jumuiya. Hii inatokea taratibu na tuna imani siku moja in shaa Allah Mungu Akipenda) tutatambulika na dunia. Na ndio maana uko hapa unafanya mahojiano hivi leo. Jamati ilianza na mtu mmoja huko katika kijiji kidogo cha Qadian India ambapo hapakuwa na barabara au gari moshi na kwa hivi sasa Jamati inapatikana katika nchi 300 duniani. Sisemi kuwa kila mtu atajiunga na Jamati Ahmadiyya na nina matumaini wanaotupinga sana wataacha.

Swali: Una ujumbe wowote kwa vijana wanaosoma gazeti hlli?
Jibu:Fikiria mfano ambao umeoneshwa na wazazi wako unapokuwa na miaka 14,15, hata 18, unaweza kufikiria kuwa umekua mkubwa na hivyo unatakiwa kuwa imara lakini lazima uzingatie yale uliyofundishwa na wazazi wako. Kinachotakiwa ni kumfahamu Muumba wako na kuheshimu mafunzo aliyotoa. Muda wako uutumie vizuri na sio kila mara uko kwenye mtandao. Kwenye michezo na ukipoteza pesa jaribu kufikiria juu ya Muumba wako, madhumuni ya dini, wajibu wetu kwa Allah. Fikiria maisha katika nyanja hizi na kwa njia hiyo tunaweza kuwa na jamii bora katika nchi yako na dunia yote kwa ujumla.

Katika mahojiano mtukufu Khalifatul Masih wa V atba alisema Waalimu wengi wanategemea wastashirikina(orientalist) kuhusu Islam na wategemee vitabu vinavyoaminika vitabu alivyo washauri waalim wa RE wavisome ni hivi vifuatavyo:-
1. Introduction to the study of the Holy Qur'an, www.alislam.org/library/books/Introduction-study-Holy-Quran.pdf
2. ◎The life and character of the Seal of the Prophets:
-Volume 1, www.alislam.org/book/life-character-seal-prophets-vol-1/
-Volume 2, www.alislam.org/book/life-character-seal-prophets-vol-2/
-Volume 3, www.alislam.org/book/life-character-seal-prophets-vol-3/
3. The economic system of Islam, www.alislam.org/book/economic-system-islam/
4. ◎The philosophy of the Teachings of Islam, www.alislam.org/library/books/Philosophy-of-Teachings-of Islam.pdf

ZIARA YA AMIR SAHIB

NA JALSA SALANA YA MKOA WA IRINGA

Kutoka Uk> 01

Mkuu wa Mkoa kwamba, Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya ilianzishwa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. wa Qadian-India, (1889) aliyeutangazia ulimwengu kwamba Mwenyezi Mungu amemtuma kuwa Masihi na Mahdi kwa ajili ya umati wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. katika zama hizi za mwisho. Na baada ya kufariki kwa mwanzilishi wake mtukufu, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. (1835-1908). Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani ilipata mfumo mpya wa uongozi wa Ukhalifa, ambapo Khalifa anayefuata huchaguliwa mara tu Khalifa aliyemtangulia anapofariki.

Akasema kwa sasa Jumuiya inaongozwa na Khalifa wa Tano wa Masihi Aliyeahidiwa a.s., Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) anayeishi nchini Uingereza kutokana na hali ya uhuru wa ibada kuwa tete huko Pakistan. Naye Amir Sahib akasema kuwa muda wa miezi kama mitano iliyopita ameteuliwa na Khalifatul Masih V kuwa Amir na Mbashiri mkuu wa Tanzania.
Amir Sahib alimwambia Mkuu wa Mkoa kuwa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ni Jumuiya yenye malengo ya kidini tu, isiyo na makusudio yoyote ya kisiasa wala ya kibiashara. Daima kama taasisi Jumuiya hihaijihusishi na siasa za nchi yoyote duniani, isipokuwa waumini wake wanayo ruhusa hiyo ya kuchagua upande wowote wa kisiasa.
Amir Sahib alisema kuwa Jumuiya hii tangu isajiliwe hapa nchini mwaka 1934, Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya imeendelea kutoa mafundisho sahihi ya dini ya kiislam, ambayo yanasisitiza amani, upendo, uvumilivu, heshima na kusaidia watu wote bila kujali, kabila, imani na itikadi zao. Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya siku zote iko mstari wa mbele kushirikiana na Serikali yetu katika kuleta maendeleo ya nchi yetu pamoja na kuwahimiza waumini wake kutii Sheria za nchi.
Amir Sahib aliendelea kusema kuwa shughuli kubwa na ya pekee ya Jumuiya hii ni kuwaongoza waumini wake na wanadamu kwa ujumla kumwamini kiuhalisia Mola wao Aliyewaumba na kutimiza haki ya kumuabudu yeye pekee na pia kutimiza haki ya kuwatumikia viumbe Wake na hivyo kuchagiza uwepo wa amani na maelewano mema miongoni mwa waumini wa dini mbalimbali.

Amir Sahib pia alimueleza Mkuu wa Mkoa kuwa shughuli zinazofanywa na Jumuiya hii ni pamoja na uchapaji wa vitabu vya dini kwa lugha mbalimbali na hivyo kusaidia kutokomeza ujinga na kuleta maelewano mazuri baina ya dini zote duniani. Alieleza kuwa hapa nchini Jumuiya hii ndio ya kwanza kutafsiri Qurani Tukufu kwa lugha ya Kiswahili(1953).
Shughuli zingine zifanywazo na jumuiya yetu ni kutoa huduma za afya, elimu na Maji safi kwa watu wote bila kujali imani na itikadi ya mtu. Ambapo akatolea mifano ya hospitali yetu ya Morogoro, Shule ya Msingi Morogoro na Shule ya Sekondari ya Kitonga.

Katika Nyanja ya huduma za Maji safi, Amir Sahib alimweleza Mkuu wa mkoa kuwa Kwa kupitia shirika letu la Kimataifa la *Humanity First* (**Ubinadamu kwanza**) – ambalo hapa nchini limesajiliwa. Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya imetekeleza miradi ya uchimbaji na ukarabati wa visima vya pump za kusukuma kwa mikono na umeme wa jua zaidi ya 300 katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu n.k. ili kuwasaidia wananchi kupata huduma ya Maji safi na salama. Huduma hii ya Maji hutolewa bure, kwa watu wote bila ubaguzi wa aina yoyote. Akamalizia kwa kusema kuwa '' Kauli mbiu ya Jumuiya yetu ni "*Love For All, Hatred For None*", yaani: **Upendo kwa wote,Chuki si kwa yeyote**.
Amir sahib baada ya kumueleza hayo Mkuu wa Mkoa kisha alimkaribisha Maulana Sheikh Abdulrahman Ame naye aeleze machache kuhusiana na Jamaat. Ambapo, Sheikh Ame akasema mengi yameshaelezwa na Amir Sahib ila akasema anayo mifano michache ya waumini wa Jumuiya hii kuwa Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu hata baada ya uhuru mtu aliyebuni jina la nchi yetu "**Tanzania**" alikuwa ni muumini wa Jumuiya hii Bw. Muhammad Iqbal Dar aliyekuwa anaishi Morogoro wakati huo ila kwa sasa anaishi Uingereza.
Pia hakusita kuutaja uwanja wa Sheikh Amri Abeid uliopo Arusha kuwa jina lake limetokana na mfuasi wa Jumuiya hii ambaye aliwahi kuwa Meya wa kwanza mweusi wa DSM na Waziri katika Serikali ya Hayati Mwalimu Nyerere wakati huo.
Baada ya maelezo haya yote kuwekwa mbele ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa aliushukuru ujumbe wa Amir Sahib uliofika Ofisini mwake na kusema kuwa Serikali ya Mkoa iko pamoja na Jamaat na wakati wowote wakihitaji msaada wa Serikali yake atawasaidia.
Siku hiyo hiyo ya Ijumaa, Majira ya saa tano ya Asubuhi (5:00) Amir Sahib alifika katika ukumbi


Amir Sahib akiwa katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa-Iringa

ambao ulikuwa umeandaliwa kwa ajili ya kufanya mkutano na waandishi wa Habari *(Press Conference).*
Amir Sahib aliwaeleza waandishi wa habari kutoka Azam Tv, habari leo, Nuru Fm na Ebony Fm kuhusiana na ziara yake kwa Mkoa wa Iringa kwa siku tatu (3) atakazokuwepo. Pia, akawaeleza dhumuni la kuanzishwa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya, ikiwa ni katika kudumisha haki ya Allah na viumbe wake ikiambatana na kutoa huduma za kibinadamu

Ukurasa wa 08

Bustani ya Washairi

KUFUMBA

Siku ya macho kufumba, na miyomo kadhalika
Nikabebwa ja mtumba, mabegani kuniweka
Naomba sana Muumba, Rabi uso mshirika
Nisamehe mja wako, pale nilipoteleza.

Mahmood Hamsin Mubiru

RAHA YA MKE NI PEPO DUNIANI NA AKHERA

Bismilahi awali, awali yake Jalia,
Mkarimu wa Adili, na mja humjalia
Akatuliza akili, furaha humfikia,
Raha ya mke ni pepo, Duniani na Akhera,

Ndugu yangu wa awali, leo umeifikia
Amekujali Jalali, timiza lengo sikia
Siku hii ya awali, umepewa na Jalia
Raha ya mke ni Pepo, Duniani na Akhera.

Leo ni siku kamili, hakika imefikia,
Manani wetu Kajali, Utulivu kufikia,
Dini yake ya halali, leo waikamilisha
Raha ya mke ni pepo, Duniani na Akhera,

Oa sioe Jahili, mwenye mwendo ulombaya,
Uoe mke Jamali, Akupendeze hisiya,
Wa asili na fasili, Akutulize sikiya,
Raha ya mke ni pepo, Duniani na Akhera,

Akupendeze kwa hali, kwa umbile na tabia,
Mtambuzi wa Jalali, na yake njema sheria,
Mrembo wa yako shani, Akuenzi kwa murua
Raha ya mke ni pepo, Duniani na Akhera,

Oa mwema kwa jamii, zingatia nakwambia,
Mwovu sioe kwa asili, utakosa kutulia
Mfunze na kusali, upate kufurahia
Raha ya mke ni pepo, Duniani na Akhera,

Mfunze yalo halali, ya Akhera na Dunia,
Amjali na Jalali, kwa yake njema tabia,
Usimfunge kufuli, akawa kama mtumwa,
Raha ya mke ni pepo, Duniani na Akhera,

Ndugu yangu Kalumale, mawaidha zingatia,
Tabia yako ilenge, mwelekeo uwe mwema,
Maisha piga mshale, upate kufanikiwa,
Raha ya mke ni pepo, Duniani na Akhera,

Salaam Alaikumu na heri nakutakia
Maisha yawe matamu, mumjali na karima
Akutoleni magumu, na kizazi kiwe chema
Raha ya mke ni pepo, Duniani na Akhera,

Hapa ndugu nifikile, lakheri na kutakia
Mola mema Awajaze, shikamana na Jalia
Njema kuburi mjazwe, mpate maisha mema,
Raha ya mke ni pepo, Duniani na Akhera,

Mtunzi
Haruna R. Bundala
Kiloleni Bombamzinga
S.L.P 54
SIMU 0783251566
TABORA

YAKINI NI DAWA BORA, UNYWE KWA BISMILLAHI

Naanza kwa Jina Lake, Mtakatifu Manani,
Hakuna zaidi yake, Maliki yaumiddini,
Sisi watumishi wake, pepo yake twatamani,
Utukufu Ni Wa Kwake, Nasi Viumbe Dhaifu.

Kila atakasikaye, kwa Yakini tu kajuzu,
Dhara avumiliaye, si kirahisi kafuzu,
Idhini kishatowaye, kamwe hutobaki zuzu,
Yakini ni dawa bora, anza audhubillahi.

Twakumbushwa hatuwezi, kutoa giza moyoni,
Hadi tufanye malezi, kujijazia Imani,
Ndipo roho muenezi, atufikie bayani,
Yakini ndio baraka, madhambi iondoayo.

Kukatazika na dhambi, Yakini ndo yake nguzo,
Kama kufuta kitambi, mazoezi ndo kigezo,
Hutozikimbia dhambi, kama Yakini kikwazo,
Yakini ndo somo leo, masikio fungueni.

Piga mfano wa nyoka, aliye mwake shimoni,
Na Simba alokereka, na nyama anatamani,
Yakini itakutaka, kutofika hatarini,
Ihamishie kwa Allahsw, hutoasi duniani.

Hutoasi duniani, na utajazwa amani,
Hatokugusa shetani, atawekwa kifungoni,
Ninayowausieni, mejifunza kitabuni,
Chake Ahmadias Wangu, Mtakatifu Mkweli.

Manaswara nao sasa, kila siku watongoa,
Damu ya Nabii Issaas, dhambi imewaondoa,
Lakini wa Allahsw, Issaas, Yakini limuokoa,
Yakini ladha tukufu, iteremkayo juu.

Naapa kwa Jina Lake, Mola asiye ajizi,
Ahmadias ni wa Kwake, kamtuma siku hizi,
Kuwa kwa amri yake, awe wetu Kiongozi,
Yakini inayoishi, inauzwa kwa Mahdi.

Enyi watu mloitwa, kwenye wema na utawa,
Fahamuni mnavutwa, kwa Allahsw mwenye usawa,
Rohoze tatoharishwa, na kusafishwa madowa,
Ili kufikia hayo, moyo ujazwe Yakini.

Tusidanganyike watu, kuwa tunayo Yakini,
Wakati vitendo vyetu, kama zetu tamaduni,
Na hata miguu yetu, haielekei dini,
Yakini si mdomoni, ni vitendo na moyoni.

Yakini sio kuua, wala damu kumwageni,
Eti unajilipua, kwa ajili ya imani,
Utakuwa wapotea, kaa chini soma dini,
Yakini sio kafara, ni ukweli uthabiti.

Dini hitokuwa ile, ambayo ishara zake,
Ziwe ni visa vya kale, hewa ubashiri wake,
Wameangamia wale, lofunga ishara zake,
Ambao hawaamini, Mungu bado anasema.

Kama ladha za dunia, zipandavyo maasia,
Ladha za kiroho pia, zinavuta kwa jalia,
Hata zinakulevyia, upige chini dunia,
Yakini inatambuza, dunia ni takataka.

Mtu anaokolewa, katika madhambi yake,
Pale anapotambuwa, uwezo wa Mola Wake,
Kila asi mwalojuwa, ujinga ndo chanzo chake,
Hizo ni nywira za kambi, nakupa msisitizo.

Ndugu zangu waumini, sipende vya ardhini,
Bali turuke hewani, na kusaka vya mbinguni,
Dhambi tujihadharini, kifo hiko ki njiani,
Juhudi tusikawize, tuamini na tutii.

Tudumishe sala zote, tuombe na kusubiri,
Qur'an tuishike, sana tuitafakari,
Ili Mola atukute, twanyenyekea twakiri,
Yakini ni dawa bora, unywe kwa bismillahi.

Awavyo Mwenyezi Mungu, ndivyo alivyokuwavyo,
Hana mwanzo toka tangu, na hufanya atakavyo,
Nina Yakini na Wangu, hupenda anileavyo,
Twashukuru Mola wetu, twaomba huruma Zako.

Katuambia Rabana, hatutofika peponi,
Kama hatujafanana, na wenzetu wa zamani,
Walitetemeshwa sana, na kuishi mashakani,
Hadi wakaulizana, msaada waja lini?,

Mungu wetu mhisani, akasema sikiliza,
Waambie waumini, msada sitokawiza,
Kwa yao hiyo Yakini, Mola akawatukuza,
Yakini jama Yakini, isemwe hadithi gani?

Unadhani ni kwa nini?, atupenda atulea,
Kwetu anataka nini?, kipi twamuongezea?,
Kuna namna naamini, Allahsw atupendelea,
Tusizizike imani, tuungane na jalia.

Tamati shairi hili, nimejaribu kutunga,
Kama dozi si kamili, mimi bado ni mchanga,
Tufike hospitali, ili madhambi kufunga,
Yakini ni dawa kuu, kwa afya ya roho zetu.

Limeandikwa na Kujumuishwa nikiwa shule,
Kibiti Boys High School {2023},
Ibrahim Soud Sha'ban Jaka,
Ifakara, Morogoro.
+255 679 149 838

Kasida ya kumsifu Mtume Mohamed (saw)

25

شيئان كان القوم عمياً فيهما
حسو العقار و كثرة النسوان

Tafsiri: Watu walikuwa wamepofuka katika maovu mawili; kunywa pombe na (kuoa) wanawake wengi

Maelezo: Kabla ya ujio wa Uislamu watu wengi walizama katika upendo wa dunia na kwenda mbali na dini. Ingawa waliona kwa macho yao ya kimwili lakini walikuwa vipofu kwa macho yao ya kiroho. Pombe ilikuwa sehemu ya lazima ya maisha yao na walichukulia kama mchezo kuoa na kuachana na wanawake. Dini ya Uislamu ikaleta ustarabu kati yao.

(Shahab Ahmad)

Hadithi ya Hamasa ya Kiislamu:

Jifunze hekima na Mabadiliko

Hapo zamani za kale, mtu mmoja alipokuwa akitembea kando ya fukwe, mwanamume mzee mwenye hekima alimwona mtu kwa mbali akiinama, akiokota kitu na kukitupa baharini.
Alipokaribia, aligundua kuwa sura hiyo ilikuwa ya mvulana mdogo, akiokota samaki wa nyota mmoja baada ya mwingine na kumrudisha



kila mmoja ndani ya maji.
Mzee mwenye hekima alikuja karibu zaidi na kuita, “Habari za asubuhi! Nikuulize unafanya nini?"
Mvulana mdogo alitulia, akatazama juu na kujibu, "Kutupa Starfish nyuma ya bahari."
Yule mzee mwenye hekima alitabasamu na kusema, “Ni lazima niulize, kwa nini unatupa samaki nyota tena baharini?”
Kwa hili, mvulana mdogo alijibu, "Jua limechomoza na mawimbi yanatoka. Nisipozitupa ndani, zitakufa.”


Aliposikia hivyo, mwanamume huyo mzee mwenye hekima alisema, “Lakini, mvulana mdogo, hutambui kwamba kuna maili na maili nyingi za fukwe na kuna samaki nyota kwenye kila maili? Huwezi kuleta mabadiliko!”



Mvulana huyo alisikiliza kwa upole. Kisha akainama, akaokota samaki mwingine wa nyota, akamtupa tena ndani ya bahari kupita yale mawimbi yaliyokuwa yakipasuka na kusema, “Ilifanya tofauti kwa huyu.”

Mara nyingi tunafikiri sisi si wa maana sana au sio muhimu sana kuleta mabadiliko. Hatukuweza kuwa zaidi kutoka kwa ukweli. Kwa hiyo, ninaweza kukuhimiza kuchukua muda wa kufanya kitu ambacho kitafanya mabadiliko kwa maisha ya mtu mwingine na sio lazima kuwa mengi na hawana haja ya kujua. Chukua muda kidogo, fanya kitu maalum, ulimwengu utajua na hiyo inatosha.
mimi ni mmoja tu; lakini bado mimi ni mmoja. Siwezi kufanya kila kitu, lakini bado ninaweza kufanya kitu; Sitakataa kufanya kitu ninachoweza kufanya. - Helen Keller
Mtu hajazaliwa ulimwenguni kufanya kila kitu bali kufanya kitu. - Henry David Thoreau

Unganisha Nukta kupata Mchoro



JIFUNZE KUPIKA KEKI YA NUSU KILO

Vinavyohitajika

- Siagi ya baking 250g – robo kilo.
- Sukari 250g – robo kilo.
- Unga wa ngano 500g –nusu kilo.
- vanilla kijiko 1 cha kulia chakula.
- Baking powder kijiko 1 cha kulia
- Mayai 6-8

JINSI YA KUTAYARISHA

Weka siagi ndani ya bakuli la kuchanganyia



pamoja na sukari uichanganye pamoja mpaka vichanganyike vizuri (unaweza kuisaga sukari yako ukitaka lakini si lazima).

Ikichanganyika vizuri weka yai moja moja uchanganye pamoja pia ichanganyike vizuri.

Anza kuweka unga kwenye mchanganyiko wako Hakikisha unaweka unga wako kidogo kidogo alafu unachanganya na sio wote kwa wakati mmoja.
Weka vanila kijiko kimoja na uchanganye kidogo kisha weka baking poda yako na uchanganye. Baada ya hapo mchanganyiko wako utakua tayari kwa kuokwa..

ZINGATIA

Unaweza kutumia mashine ya kusagia keki na kama huna tumia mwiko tu kwa kuchanganyia na itakuwa nzuri tu usikhofu.

ZIARA YA AMIR SAHIB

NA JALSA SALANA YA MKOA WA IRINGA

Kutoka Uk> 05

bila ya kuangalia imani za watu. Na bilkhususi akasema kuwa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ni Jumuiya yenye malengo ya kidini tu, isiyo na makusudio yoyote ya kisiasa. Daima kama taasisi Jumuiya hii haijihusishi na siasa za nchi yoyote duniani, isipokuwa waumini wake wanayo ruhusa hiyo ya kuchagua upande wowote wa kisiasa.

Baada ya hapo waandishi wa habari waliuliza maswali mbalimbali yahusuyo maadili na kutaka kujua msimamo wa Jamaat juu ya ukatili wa watoto, masuala ya ndoa za jinsia moja na namna ya kuwainua watu kiuchumi.

Amir Sahib alisema “Kupitia misingi wa dini ya Kiislam, tunafundishwa kuishi kwa amani, upendo, kuheshimiana, na kuvumiliana na watu wa dini nyingine pamoja na jamii nzima. Tumekuwa tukifanya mikutano ya amani katika mikoa mbalimbali nchini ili kueneza ujumbe huu,” Amir Sahib alitoa wito kwa jamii kuweka mkazo kwenye malezi bora na maadili kwa watoto ili kujenga kizazi chenye ustawi na kuzingatia heshima na maadili ya dini. Alisema kuwa malezi ya vijana ndiyo msingi wa kuunda jamii yenye kumcha Mungu na yenye uwezo wa kupambana na kuondoa ukatili, mmomonyoko wa maadili na tabia zisizoendana na maadili mema.

Kuhusiana na ndoa za wapenzi wa jinsia moja Amir Sahib alisema “dini ya Kiislam ambayo ni dini yetu na sisi Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya hatuungi mkono na fikra hiyo ya ndoa za Jinsia moja. Kurani Tukufu inaenda kinyume na fikra kiyo. Katika Kurani Tukufu tunaona baadhi ya mataifa yaliyofanya masuala hayo yaliangamizwa.”

Akizungumza kuhusu masuala ya maendeleo, ajira, na ujasiriamali kwa waumini, Amir Sahib aliwahimiza vijana kujituma katika elimu na kupata ujuzi ambao utawasaidia kupambana na changamoto za kiuchumi na hivyo kuondokana na umasikini. Alisema kuwa “Elimu ni ufunguo wa maisha. Watanzania na waumini wetu wakiwekeza kwenye elimu, hiyo ni njia bora zaidi ya kukabiliana na changamoto za maendeleo kwa ujumla,”. Akakazia kwa kusema ukatili wa watoto ni pamoja na kutowapa elimu na maezi bora.

Mazungumzo na waandishi wa habari



Mara baada ya Sala ya Ijumaa majira ya Saa tisa Alasiri, Jalsa salana ya Mkoa ikaanza rasmi ambapo Maulana Amir Sahib alifungua kwa maombi kisha akatoa hotuba iliyohusu madhumuni ya Jalsa Salana kama yalivyoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Na Majira ya Saa kumi za Alasiri washiriki wote walifanikiwa kufuatilia hotuba ya Huzur wakiwa katika ukumbi wa mkutano. Hotuba ya Huzur kuhusuana na Tahrik Jadid ikatolewa na mpendwa wetu Huzur a.t.b.a huku watu wakifuatilia MTA kwa lugha ya Kiswahili katika ukumbi wa mkutano.

Kulingana na Ratiba ya Jalsa Salana, majira ya saa 11:00-12:30 ulikuwa wasaa mzuri sana kwa Tanzim zote 3 kuweza kukaa na kujadiliana na wanachama wao juu ya maendeleo ya Tanzim husika. Ambapo, Viongozi na ndugu zetu wa kutoka Dar es Salaam waolifika walichagiza vikao hivyo katika majadiliano.

Wakati wa Usiku mara baada

Ukurasa 09

Maelekezo ya maisha katika Qur'an

31_ Toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu (56:7)

32_Jihimizeni kuwalisha maskini (107:7)

33_ Watafuteni wenye kuhitaji muwasaidie (2:283)

34_Usitumie ovyo pesa zako (17:29)

35_Msiharibu sadaka zenu kwa masimulizi (2:264)

36_ Wakirimu wageni (51:26)

37._Waamrishe watu kutenda mema baada ya wewe mwenyewe kuyatenda (2:44)

38_Msifanye uharibifu katika Ardhi (2:60)

39_Msiwazue watu kuingia misikitini (2:114)

40_Piganeni na wale wanaowapigeni tu (2:190)

MATUKIO KATIKA PICHA

ZIARA YA AMIR SAHIB

NA JALSA SALANA YA MKOA WA IRINGA

Kutoka Uk.08

ya sala ya Magharibi na Isha tulipata bahati ya kufanya kipindi cha maswali na majibu ambapo Amir Sahib pamwe na wabashiri walioambatana naye walishiriki kipindi hicho na maswali mbalimbali kutoka kwa wanawake kwa wanaume yakaulizwa. Mfano wa swali moja wapo lililoulizwa ni juu ya Wanajamaat kuoa au kuolewa nje ya Jamaat. Majibu yaliyotolewa ni kwamba kufanya hivyo ni Usaliti kwa Amri ya Khalifa wa zama.

Kipindi cha Maswali na Majibu



Siku ya Pili 09/11/2024 anga likiwa angavu kabisa mara baada ya Sala ya Tahajud na Alfajiri tuliendelea na ratiba ya Jalsa Salana katika ukumbi wa Siasa ni Kilimo uliopo jirani kabisa na Msikiti wetu hapa Iringa Mjini.

Ambapo tulipata ugeni wa Mkuu wa Wilaya (DC) Mh, Herry James na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Iringa Mh, Ibrahim Ngwada. Viongozi hawa walifika kwa pamoja na kusalimiana na waumini waliokuja kushiriki Jalsa Salana.

Amir Sahib akimkabidhi zawadi ya



Kurani Tukufu Mh. DC Herry James



Amir Sahib akimkabidhi zawadi ya Kurani Tukufu Mh. Mstahiki Meya, Ibrahim Ngwada



Mh. DC, Herry James akipokea maelezo kwenye banda la maonesho

Baadaye pia tulipata Baraka za ujio wa Diwani Mstaafu wa kata ya Gangilonga ambapo ni eneo Msikiti wetu ulipo. Ndugu, Leonard Mgina, yeye pia ni msaikolojia na alieleza machache kuhusiana na ujumbe wetu wa amani na namna saikoloji inavyotaka kusameheana ili kupata amani ya mwili



Mh. Ndugu, Leonard Mgina akipokea zawadi kutoka kwa Amir Sahib

Baada ya wageni kuondoka tuliendelea na mada zetu za Jalsa Salana ambapo Maulana Sheikh Asif Mahmood Butt Sahib alizungumzia juu ya Wajibu wa Mume na Mke katika maisha ya ndoa. Naye Maulana Sheikh Abdulrahman Ame alizungumzia wajibu wetu katika kudumisha Nidhamu ya Ukhalifa. Na mwisho alikuwa Maulana Sheikh Asif Raza Sahib ambapo hotuba yake ililenga kwenye kujitolea Mali katika njia ya Allah.

Mwisho Amir Sahib alitoa hotuba na akafunga kwa kufanya maombi ya kimya kimya na hapo ikawa ndio mwisho wa Jalsa Salana yetu, Alhamdulillah. Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu, Jalsa hii ya mkoa ilihudhuriwa na watu 292 (Wanaume 166 na Wanawake 126) kutoka matawi yote ya Mkoa wa Iringa na wageni 40 kutoka nje ya Iringa.

Mimi kama Afisa Jalsa Salana ya Iringa kwa mwaka huu, natoa shukrani zangu kwa wanakamati wote waliohudumu, Allah awapokee juhudi zao, Amin. Bila ya kuwasahau Wanajamaat kutoka Mkoa wa DSM waliokodi gari (Costa) iliyokuja katika Jalsa ya Iringa ambapo ujio wao uliamsha ari na kutoa msaada mkubwa katika kamati za Jalsa Salana yetu. Allah apokee juhudi zao, Amin

Jioni majira ya saa kumi Alasiri (10:00) Amir Sahib alifanya kikao na viongozi mbalimbali katika Makao makuu yetu ya Jamaat hapa Iringa na kubadilishana nao mawazo juu ya uongozi na



Picha ya Pamoja ya kufunga Jalsa Salana ya Iringa

kuweza kubaini changamoto mbalimbali.

Na ilipofika majira ya saa kumi na moja na nusu jioni Amir Sahib na ujumbe wake waliongozana na viongozi wa Jamaat wa Iringa kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa Ukarabati wa Msikiti wa Mtwivila na ujenzi wa Msikiti wa Mkwawa. Ambapo, aliwaagiza viongozi kufanya tathmini na kuona kama siku za baadaye anaweza kusaidia tena kwa ajili ya kumalizia kazi hizo. Aidha kwa upande wa Msikiti wa Mkwawa, aliwapongeza wanajamaat kwa kujitolea kujenga msikiti mzuri na kutaka siku zijazo kuweka taarifa vizuri za shughuli za ujenzi kwa kumbukumbu za kiofisi.



Picha ya Pamoja ya tawi la Mtwivila



Amir Sahib akikagua Msikiti wa tawi la Mkwawa

Amir Sahib alipokuwa tawi la Mkwawa aliweza kukutana na Mwanajamaat Mkongwe zaidi hapa Iringa akikadiriwa kuwa na miaka zaidi ya 102.

Picha ya Pamoja na Mzee Daud Mkeremi



Tarehe 10/11/2024 Msafara wa Amir Sahib ulianza ziara ya kutembelea baadhi ya matawi ya Jamaat kwa maeneo ya Izazi na Magozi. Majira ya saa tatu msafara wake ukaanza kuondoka kwenda Izazi tawi lililopo Km kama 90 kutoka Mkoani Iringa.

Mara baada ya kufika Izazi, Amir Sahib alikagua ukarabati wa Msikiti na ujenzi wa nyumba ya Mwalimu. Kwa ambao tunaopajua Izazi, tulikutana na mabadiliko makubwa ya Mandhari nzuri ya Msikiti na nyumba ya Mwalimu kutokana na ukarabati huo uliofanyika. Na mara baada ya ukaguzi tuliingia msikitini kwa ajili ya kikao na wanajamaat wa tawi hilo.

Risala ilisomwa ya tawi na salamu mbalimbali za viongozi wa tawi na Serikali kupitia Mtendaji wa Kijiji hicho. Na kisha Amir Sahib alimwalika Sadr Khuddam, Sheikh wa Mkoa na Maulana Sheikh Ame kusema machache kabla ya kuanza nasaha zake kwa wanajamaat.

Kisha Amir Sahib aliwapongeza sana wanatawi hilo kutokana na kusimamia ukarabati wa msikiti na akawahimiza kufanya Tabligh kwa wingi ili kuongeza idadi yao iliyopo sasa 52. Kwa kuwa Tawi hili liliasisiwa mwaka 1998 na hivyo, akasema miaka 26 imepita hivyo wajitahidi kufanya mahubiri zaidi ya hapo.



Picha ya Pamoja na Wanajamaat wa tawi la Izazi

Maswali kutoka katika kitabu cha

MHISANI KWA UBINADAMU

Imetayarishwa na.
Sheikh Ali Dino Tahir - Simiyu

Uk. 31 31. Hadhrat Aisha RA alisemaje kuhusu Khulka za Mtume SAW
Jb. Hadhrat Aisha R.A. alisema KANA KHULUKU HULKURAN كان خلقه القرآن sifa zote zenye kusifika zilizomo ndani ya Kurani Tukufu zote zilipatikana ndani mwake.

32. Kwanini Hadhrat Aisha RA alikuwa analia wakati wa kula chapati ya unga wa ngano safi.
Jb. Kwa sababu yeye hakuweza kumtayarishia Mtume SAW chapati ya unga wa ngano safi bali alikuwa anakula ngano iliyosagwa na mawe nyumbani.

Uk.32 33. Badhi ya masahaba walimpa ushauri gani Sayyidina Abubakari RA kuhusu lile jeshi ambalo Mtume saw aliliteua kwenda vitani kabla ya kufariki kwake.
Jb. Baada ya kufariki kwa Mtume Muhammad SAW watu wengi waliasi na kukataa kutoa kodi. Masahaba walimuambia kwanza inabidi kukabiliana na watu hawa, hivyo lile jeshi ambalo Mtume saw aliliteua kwenda vitani kabla ya kufariki kwake lizuiliwe ; kwanza tukabiliane na uasi wa ndani kisha jeshi lile litumwe.

34. baada ya kufariki kwa Mtume[saw] Sayyidina Abubakari radhiallah anhu alisemaje kuhusu jeshi lile la Usama bin Zaid ra kutumiwa kwao vitani, jeshi ambalo Mtume saw aliliteua kwenda vitani?
Jb. Ndani ya moyo wa Hadhrat Abu Bakar radhiallah anhu ilikuwa na heshima kubwa sana ya Mtume kiasi hiki kwamba alitaja jina la baba yake kwa kusema: Je mwana wa Ibnu Abi Kahafa anao uwezo huu kwamba alizuie (kwenda vitani) jeshi lile lililoagizwa na Mtume? Kwa haki ya Mwenyezi Mungu, hata kama adui aje Madina na kuwaburuza wanawake wetu, basi hata hivyo sintolizuia jeshi lile.

35. Baada ya kufariki kwa Mtume Muhammad saw kauli yake ikawa na umuhimu mkubwa kabisa kwa wafuasi wake, jambo hili linathibitisha nini? Jb. Jambo hili linathibitisha kwamba Mtume Muhammad SAW alikuwa Mkweli kabisa

Uk.33 36. Hadhrat Umar RA khalifa wa pili aliomba nini kwa Bi Aisha kabla ya kufariki kwake
Jb. Alimuomba Bi Aisha RA kwamba kama yeye ataruhusu basi anaomba azikwe pembeni mwa kaburi la Mtume

Uk.34 37. Hadhrat Uthman RA Khalifa wa tatu alishauriwa nini wakati watu waasi walitaka kumuua na yeye alifanya nini
Jb. Katika zama za Uthman kulitokea uasi na waasi wakaja kumuua. Wakati huo Hadhrat Muawya alimjia na kummpa ushauri huu ,kwa kuwa waasi wana dhamiria hivi kwamba baada ya kukuua watamuweka sahaba mwingine kuwa Khalifa;Hivyo wapeleke nje wale Masahaba wakubwa kukulinda,lakini Hadhrat Uthman RA hakukubali ushauri wake.

Uk. 35 38. Ushahidi gani unakuwa sahihi kuhusu mtu yeyote
Jb: Ushahidi wa mke wake, na Ushahidi wa watu wa zama zile zile waliomuona na kuishi karibu yake

39. Katika vita gani Mtume Muhammad SAW na masahaba wengi walijeruhiwa? Jb. Vita vya uhudi

Uk: 36 40. Kwanini Mtume Muhammad SAW alikuwa anawazuia masahaba wake waitikie walipokuwepo nyuma ya mlima katika vita vya Uhudi. Jb. Kwa sababu wakati ule masahaba wengi walijeruhiwa na kulikuwa hatari isije makafiri wakawageukia tena kuwashambulia.

41. Abujahali aliposema u'ulu hubal u'ulu Hubal yaani shani ya sanamu Hubal iwe juu, kwanini Mtume aliwaambia masahaba wake watoe jibu kwa sauti kubwa hali walikuwa hatarini.?
Jb. Mtume Muhammad SAW aliwaambia wakae kimya kwa sababu ya uhai wao lakini walipoanza kuitukuza sanamu yao na kumdhalilisha Mwenyezi Mungu, Mtume hakuweza kuvumilia.

42. Mtume Muhammad SAW aliwaambia nini kuwajibu makafiri walipoanza kulitukuza sanamu lao ?
Jb.Mtume Muhammad SAW aliwaambia waseme kwa sauti kwamba Allahu Aala wa ajal.

43. Nini maana ya Allahu Aala wa ajal Jb. Mwenyezi Mungu tu ndiye mwenye heshima na mwenye shani
Uk. 37 44. Tauhid ni nini? Jb. Umoja wa Allah Mtukufu.

45. Masahaba walipotoa Jibu kwamba Allahu aala wa ajal, je makafiri waliwashambulia tena.
Jb. Hapana, waliogopa walidhani kwamba katika hali hii wanatoa jibu kwa ujasiri huo,bilashaka hao wameshaandaa kutuua, wakakimbia.

Uk. 38

46. Kwa sababu gani wema wa Sayyidna Abubakari, Sayyidna Umar, Sayyidna Uthmani na masahaba wengine Mungu awe radhi nao wote ni dalili wa utakatifu wa Mtume SAW?
Jb. Kwa sababu walikuwa wanafunzi wake ; Mtume aliwalea , kama wao wote ni wema na wazuri lazima mlezi wao atakuwa mzuri zaidi kuliko wao.

47. Khalifa gani aliishi nyumbani mwa Mtume SAW tangu utotoni?
Jb. Sayyidina Ali RA

Uk. 39
48. Kwanini Mayahudi na wakristo wa Sham walitaka waislam waendelee kuwatawala badala ya wenzao wakristo
Jb.Kwa sababu chini ya himaya yao mali na heshima zao zililindwa kwa kila namna.

49. Kamilisha sentensi... Kama ndani ya Muhammad SAW mngekuwa hamna utakatifu usio wa kawaida,
Jb. basi asingekuwa na uwezo wa kuwatakasa wengine

50. Mtume Muhammad SAW alipokuja, waarabu walikuwa na utamaduni gani
Jb. Walikuwa wakiona fahari katika kufanya ujambazi, kucheza kamari, na kunywa pombe
Uk 42,43
51. Ni nani aliyeharamisha kabisa pombe. Jb. Mtume Muhammad SAW
Uk 44
52. Mtume Muhammad SAW alipodai utume alikuta mazingira gani. Jb. Alipodai kwamba Mungu ni mmoja akakataza kuabudu sanamu na kutia kasoro ktk hilo washirikina wa Makka wakawa maadui zake. Aliposema Yesu ni mwanaadamu, si mwana wa Mungu bali Mungu hana mshirika, wakristo wakawa maadui zake. Na akakanusha maovu waliyokuwa wanafanya mayahudi nao wakawa maadui zake. Kwa hiyo kila mwenye dini na asiyekuwa na dini wakati wake walikuwa maadui zake na walifanya kila njama kumuua pia.
Uk. 45
53.Mtume SAW alikuwa anakula nini katika maisha yake ya kila siku?
Jb. Mke wake Mtume SAW bi Aisha Anasema kwamba "Mara nyingi tuliwahi kukosa chochote cha kula au tulikuwa tukipitisha siku kwa kula tende tu".
Uk 46.
54. Mtume Muhammad SAW na mke wake walikuwa wanatumia kitu gani kwa ajili ya kulala?
Jb. Walikuwa wakitumia ngozi ya mbuzi kwa ajili ya kulalia.
Uk.48
55. Mtume SAW alimuoa Bi Aisha RA, alikuwa ana sifa gani mpaka akamuowa?
Jb. Alimuoa bi Aisha kutokana na Uaminifu, utawa, na ucha mungu wa baba yake, naye alikuwa ana sifa za baba na kumbukumbu zuri kuliko wote wakati ule.
Uk 49,50
56. kwa sababu gani Mtume SAW aliwaambia wakeze kwamba ima waishi naye na umasikini alionao ima wachukue mali na wajitenge naye?
Jb. Mtume SAW alisema Maisha ya mwenye mali hayawezi kuyavumilia majukumu yangu ya kidini
Uk.50,51
57. Mtume Muhammad SAW alikuwa akienda kulala kwa nani kati ya wake zake
Jb. alikuwa analala kwa kila mwanamke sawa na zamu yake bila ya kumchagua hata mmoja, alikuwa mwadilifu wa hali ya juu, isipokuwa alipoumwa, wake zake walimuomba apumzike kwa Bi Aisha RA.
Uk. 51
58. Mtume SAW alipokuwa akienda kulala kwa wake zake, mara nyingi alikuwa anafanya nini
Jb. Alikuwa akipumzika kidogo na kuamka na kufanya ibada kwa masaa mengi hadi miguu yake ilikuwa inavimba kwa sababu ya kusimama muda mrefu katika sala za nafali.
Uk.51,52
59. Mtume aliwaoa wake wengi kwa lengo gani, toa ushahidi kwamba hakuoa kwa ajili ya anasa na starehe yake
Jb. 1 Mtume Muhammad[saw] hakuoa katika ujana wake isipokuwa mke mmoja na yeye alikuwa mjane na mkubwa miaka 15 zaidi kuliko yeye. 2.Aliowaoa wake zake wote walikuwa ima wajane au waliopata talaka kwa waume zao ili wao wapate kujistri na kujifunza mambo ya dini na kushika tabia yake tukufu ili waweze kuwafundisha wake za watu 3.hakuchagua vigori wala warembo na kuwaacha wake zake alipopata heshima, nguvu na ufalme hata alipopewa ruhusa na Mwenyezi Mungu kwamba anaweza kuwataliki wote na kuwaoa awatakao, lakini hakumpa talaka hata mke mmoja, wala hakutumia ruhusa hiyo. 4. Mtume SAW alimuoa Bi Aisha RA aliyekuwa bikra (asiyeolewa kabla), si kwa sababu ya tamaa yake bali kwa uaminifu wake na ufahamu wake na uwezo wake wa kumbukumbu. Ndiye mwanamke pekee aliyehifadhi hadithi nyingi na mafundisho mengi ya Mtume SAW na kutufikishia sisi waislamu, naye aliwafundisha nyuma ya pazia masahaba wengi mpaka makhalifa baada ya kufariki Mtume SAW.Na Mtume alisema kwamba mjifunze nusu ya dini kwa Aisha ra

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

HISTORIA YA AHMADIYYA ZANZIBAR

Kutoka uk. 12

HISTORIA YA AHMADIYA ZANZIBAR.

Ninamuomba Allah (sw) Ajaaliye baraka nyingi katika utungo huu ili ulete manufaa kwangu mimi mwandishi na kwa wasomaji wote, Amin.

KWA JINA LA ALLAH MWINGI WA REHEMA MWINGI WA UKARIMU

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ambayo ilianzia kwenye kijiji kidogo cha Qadiyan nchini India mnamo mwaka 1889 kupitia muasisi wake Mirza Ghulam Ahmad ilianza kutiririsha wafuasi wake mapema sana nje ya Qadiyan na nje ya India, na Zanzibar ni moja kati ya zilizopata bahati yakufikiwa na maswahaba hao watukufu wa Sayidna Ahmad a.s
Eneo maarufu liitwalo Kibanda maiti lilikuwa ni milki ya swahaba wa Sayidna Ahmad(as) ambaye alikuwa ni daktari wa Sultan wa Zanzibar Humud bin Mohd aliyetawala 1896-1902, mwili uliozikwa hapo ni wa mwanawe daktari huyo. Aidha kuna eneo lijulikanalo kama kaburi kikombe kuna kaburi maarufu linalosadikiwa kuwa ni kaburi la sharifu. Baadhi ya watu hufanya ziara kwenye kaburi hilo kwa ajili ya kuomba haja zao mbalimbali. Kaburi hili pia linasadikiwa kuwa mwili uliolazwa hapo ni wa Ahmadiyya wa zamani miongoni mwa Waahmadiyya wa mwanzoni kabisa.

Walikuwepo Waahmadiyya wengine zaidi ya hao wawili ingawa imetuwia vigumu kupata majina yao. Daktari wa sultani ndiye aliyekuwa Rais wa tawi hilo ambapo swahaba wa sayidna Ahmad, Sheikh Hafidh Hamoud Ally[ra] alidhamiria kulizuru. Sheikh Hafidh Hamoud Ally[ra] jahazi ilipofika Mombasa alishuka na jahazi hiyo ilizama wakati ikielekea Zanzibar. Habari zilienea katika Qadian ya kwamba swahaba wa Sayidna Ahmad[ra] Sheikh Hafidh Hamoud Allay[ra] amezama lakini Sayidna Ahmad (as) alisema hapana na kweli maelezo ya baadae yalikuja kuthibitisha ya kwamba alishuka kabla ya jahazi kuzama. Waahmadiyya hao wa mwanzo wote walikuwa waasia (wahindi) na waliondoka Zanzibar kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Mahubiri yao hayakuwafikia wazawa (wazanzibari) kwa sababu mbili. Kwanza lugha, kwani Kiswahili kilikuwa bado hakijakolea. Kikwazo cha pili uadui wa mashekhe waliokuwepo wakati ambao walishajazwa kasumba kwamba Waahmadiya si waislamu.

MAHUBIRI RASMI

Maswahaba wa Sayidna Ahmad walifika Afrika ya Mashariki kwa ajili ya ujenzi wa reli tokea mwaka 1896 hadi 1936 walituma maombi kwa Khalifa wa pili Hadhrat Mirza Bashirdun Mahmoud Ahmad[ra] yakupatiwa mbashiri ili kuja kuwalea Waahmadiya waliokwisha patikana na kuwaweka kwenye nidhamu ya Ukhalifa. Mnamo mwaka 1934 Khalifa mtukufu wa pili Hadhrat Mahmoud[ra] alimtuma Sheikh Mubarak Ahmad kuja kutoa huduma Afrika ya Mashariki. Sheikh Mubarak Ahmad akianzia Mombasa alifanya kazi Afrika ya Mashariki yote na kuweka kambi yake Tabora. Mwaka 1936 alianzisha gazeti "MAPENZI YA MUNGU" na mwaka 1953 alitoa tafsiri ya Quran tukufu kwa lugha ya Kiswahili.

Katika ukurasa wa 50 wa kitabu HISTORIA YA AHMADIYA TANZANIA tunasoma:- "Nakala ya nne ya Kurani Tukufu alipelekewa sultani wa Zanzibar Sir Khalifa bin Haroub" Aidha mwandishi wa kitabu hicho Muadham Mahmoud Hamsin Mubiru anatueleza kwamba sultani wa Zanzibar mtajwa hapo juu alipewa zawadi ya tafsiri ya Quran tukufu mkononi kwenye ujumbe ulioongozwa na sheikh Mubarak Ahmad mwaka huo huo wa 1953. Aidha Sultani huyu Khalifa bin Haroub ndiye aliyepewa mwaliko wa ufunguzi wa msikiti wa mjini Tabora (Alfazal) mnamo mwaka 1944, na aliupokea mwaliko huo kwa furaha ila hakuwahi kuhudhuria kwa kusema: "Zanzibar ilikuwa katika kilele cha sherehe za Abdul Said kutimiza miaka mia mbili ya utawala wake nchini Zanzibar" (Historia ya Ahmadiya Tanzania uk 71)

WAPINZANI WA AHMADIYA WAJITOKEZA

Upinzani dhidi ya Manabii wa Mwenyezi Mungu ni sunna Mu'aqqada hivyo Ahmadiya nayo ni lazima ipite katika tanuri hili kama ambavyo dhahabu hupita kwenye tanuri kabla ya kutengenezwa pete, mkufu n.k Sheikh wa kwanza aliyejitokeza hadharani kwa Zanzibar ni Sheikh Abubakar Bakathiri ambaye enzi yake aliwika sana Zanzibar. Yeye alitangaza kwamba tumeingiliwa na adui mkubwa wa Uislamu Afrika ya Mashariki ambaye ni sheikh Mubarak Ahmad, na kwamba yeyote atakayesaidia katika kuvunjilia mbali juhudi za sheikh Mubarak atapata malipo yasiyokwisha.

Sheikh huyu Bakathir alihamasisha sana watu waichukie Ahmadiya ndani na nje ya Zanzibar. Lakini upinzani kwa Ahmadiya ndio mbolea. Upinzani wa Sheikh Bakathir ulijibiwa papo kwa papo kwa majibu moto moto hadi wanafunzi wa sheilkh Bakathir wakaona haya. Sheikh huyu aliyekuwa akiheshimika sana Zanzibar alianza kudhalilika na kusawijika na hatimaye kusahaulika kabisa.

SHEIKH FARSY AFATA NYAYO

Aliyefuata nyayo za Bakathir ni Sheikh Abdalla Saleh Farsy. Yeye alitumia njia nyingi kama vile radio(sauti ya Unguja) vijarida, magazeti na vitabu. Aliandika kitabu alichokiita "UPOTOFU WA TAFSIRI YA MAKADIANI" ambacho kilijibiwa na Hayati Sheikh Kaluta Amri Abeid. Majibu ya kitabu hicho cha Sheikh Farsi ni "UONGOFU WA TAFSIRI YA KURAN TUKUFU". Kitabu hichi kimekata kabisa kidomo domo cha Sheikh Farsi.

Wakati huo Zanzibar kulikuwa na umoja fulani wa vijana ambao wao waliona ipo haja pande mbili zifanye mjadala kwa lengo la kuwapa fursa wasikilizaji ya kupima na kujua upande upi wenye hoja zenye mashiko. Ombi lao lilikubaliwa na tarehe ya mjadala ilipangwa, mahali ni Zanzibar. Siku ya mjadala ilipofika Sheikh Mubarak alimtuma mwanafunzi wake Sheikh Kaluta Amri Abeid amwakilishe. Waliokwenda uwanja wa ndege kumpokea mgeni walishangaa kumuona kijana mwafrika aliyevaa suti na brifkes ndogo mkononi. Walitarajia kumuona Sheikh mwenye majoho na kilemba. Walimpokea kwa heshima na kumfikisha mahali husika ambako alimkuta mwenyeji wake Sheikh Abdallah Saleh Farsy. Sheikh Kaluta alimkabidhi Sheikh Saleh Abdalla Farsy barua kutoka kwa Sheikh Mubarak. Aliipokea na kusoma. Ilikuwa imeandikwa "Kutokana na udhuru ulionipata nimemleta kijana Mwafrika mwenzio Kaluta Amri Abeid, ukimshinda huyo jua kwamba umeishinda Ahmadiya dunia nzima."

Baada ya kuisoma barua ile Sheikh Farsy nguvu zilimwisha na hakuwa na haja tena ya mjadala. Waliohudhuria walikuwa na hamu na shauku ya kusikia hoja za kila upande lakini Sheikh Farsy alikataa kata kata kufanya mjadala. Sheikh Kaluta alirudi kwa bosi wake na kumueleza yaliyojiri.

Tukio hili liliacha athari miongoni mwa wale waliolishuhudia, wapo waliolisimulia kwa hisia baadae wapo waliotafuta ukweli na wapo waliojiunga na Ahmadiya baadae. Sheikh Farsy akawa amepata pigo jingine. Lakini Sheikh huyu mwenye roho ngumu hakuishia hapo.

Baada ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, Sheikh huyu alihama Zanzibar na kuhamia Kenya, akiwa huko Kenya alitoa tafsiri ya Kuran tukufu kwa lugha ya kiswahili kwa lengo la kuipiku tafsiri ya Sheikh Mubarak bila mafanikio. Alichokifanya ni mkusanyiko wa matusi kuwatukana waahmadiya. Miongoni mwa alama za wanafiki moja ni kwamba anaposhindana hutumia matusi kwa kauli ya Mtume (saw).

Bakora aliyochapiwa Sheikh Bakathir ikatumika tena kumchapa Farsy. Alidhalilika yeye na alichokianzisha. Kule Kenya alitokea Sheikh aliyetunga kitabu "FIMBO YA MUSA" katika kitabu hicho alikosolewa sana sheikh Farsy kwenye elimu yake hadi ikaonekana kumbe sheikh Farsy licha ya kuitwa sheikh hafai hata kuitwa mwanafunzi.

ITAENDELEA TOLEO LIJALO IN SHAA ALLAH

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi Yangu Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE






MATUMAINI YA AMANI DUNIANI

HABARI UK> 04

HISTORIA YA AHMADIYYA ZANZIBAR



Na Ali Hamis Juma-(Majani) kiutamaduni na kielimu. historia inatueleza kwamba kuwafurusha wareno. Hata Ustaarabu wa Zanzibar unajulikana duniani kote miaka mingi kabla ya ukoloni. Kiuchumi, bandari ya Zanzibar ilikuwa ndio bandari kuu Afrika ya Mashariki. Ama kielimu, ilikuwa msomi mzuri ni yule aliyesoma Zanzibar hususan elimu ya dini ya kiislamu. Yeyote aliyediriki kupata elimu Zanzibar aliheshimika na kupewa cheo cha juu. Aidha kanisa la kwanza kabisa Afrika Mashariki ni lile la Mkunanzini mjini Unguja.

Ama kisiasa Zanzibar iliingia kwenye siasa mapema sana tangu utawala wa Bi Mwana na Mwana wa Mwana pale Wareno walipojaribu kuitawala Zanzibar kimabavu. Kwa msaada kutoka serikali ya Oman wazanzibari waliweza kuwafurusha wareno. Hata hivyo ingawa Zanzibar iliepuka utawala wa kireno ilijikuta ikiingia kwenye ukoloni wa Waarabu. Waingereza pia waliitawala Zanzibar kwa amri ya umoja wa Mataifa na kuifanya Zanzibar kutawaliwa na mabwana wawili. Waarabu na Waingereza.



Historia ya Ahmadiyya Zanzibar inaanzia kwenye kipindi hiki cha tawala za Waarabu na Waingereza yaani karne ya 19 na 20 Miladiya. Hamu ya kuandika utungo huu niliipata baada ya kusoma kitabu "HISTORIA YA AHMADIYA TANZANIA" utunzi wa Muadham Mahmoud Hamsini Mubiru. Katika kitabu hicho, Zanzibar ambayo ni sehemu ya Tanzania, imetajwa kwa uchache sana, ndipo likanijia wazo la kuandika walau maelezo machache kuhusu

Makala hii ya historia. Bila shaka yapo mengi ambayo huenda ikawa Mwandishi yamemponyoka. Tutafurahi kupata chochote kitakachosaidia kuelewa vizuri historia ya visiwa hivi maarufu katika Afrika.

UTANGULIZI

Zanzibar ni nchi maarufu sana duniani, kisiasa, kiuchumi,

HABARI UK> 11

FORTY SAYINGS OF THE HOLY PROPHET S.A.W.

By Sheikh Muhammad Munawwar H.A.
The book contains 40 short Sayings of the Holy Prophet s.a.w. and ment for children.

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

HADITHI AROBAINI
ZA
MTUME MUHAMMAD
s.a.w.

JUMUIYA YA WAISLAMU WA AHMADIYYA TANZANIA



Je, Wajua?

Watu hupepesa macho mara chache sana wanapotumia kompyuta ikilinganishwa na wakati wanasoma kitabu au kutazama TV.

Marie na Pierre Curie walikuwa wanandoa wa kwanza kushinda Tuzo ya Nobel. Walishinda kwa pamoja tuzo ya Fizikia mwaka wa 1903 kwa kazi yao ya radioactivity.

Mwanamama Marie Curie ndiye mtu pekee aliyeshinda Tuzo za Nobel katika nyanja mbili tofauti za kisayansi: Fizikia mnamo 1903 na Kemia mnamo 1911.

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 1,000/=.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com